# Maoni kuhusu makala ya F.E.M.K. Senkoro "Sanaa, Ubunifu na Jamii katika Nadharia na Fasihi"

J.S.Madumulla

1. Makala hii ina uzuri wa aina yake. Ina jambo la kusema; na ina mtiririko mzuri wa mawazo. Inabainisha mambo bayana mawili hivi. La kwanza, inaonyesha kuwa Fasihi ya/katika Kiswahili inaanza kupata ukomavu wa mikabala na mbinu za kihakiki kwa lugha ya Kiswahili. La pili, ni kuhusu mhakiki mwenyewe ambaye amesimama mahali palipoinuka katika safari yake ndefu ya kihakiki, akajipa fursa ya kuzitalii tahakiki zilizopita - za wengine na za kwake mwenyewe - na kubaini upungufu wake yeye binafsi kama mhakiki na ule wa wahakiki wengine.

2. Katika mengi ayasemayo mwandishi, mkazo ameuweka katika namna fasihi kama kazi ya sanaa ilivyoangaliwa na wahakiki hao, na dhima kubwa ambayo fasihi hiyo ilibebeshwa nao. Anaona kuwa fasihi haikustahili baadhi ya sifa ilizopewa. Kwa hiyo katika makala haya, mwandishi anadai kuwa:

a) Fasihi haitawaliwi na masuala ya kiitikadi kama ambavyo ilisadikiwa awali, kwani si chombo cha kiitikadi tu;

b) Fasihi haiwezi kujitenga na jamii kama ambavyo mara nyingine imedaiwa kuwa, kwani fasihi ni zao la jamii;

c) Fasihi haiwezi kuibua maudhui mapya, wala kuleta mapinduzi, kwani haina uwezo huo. Uwezo wake uko kwenye usawiri wa mambo hayo tu;

d) Fasihi haiwezi kubuni, huunda tu ulimwengu kutokana na ule uliopo;

e) Mwanafasihi huiigiza jamii na kujiigiza mwenyewe; haziundi hali hizo;

f) Fasihi si silaha (k.v. ya mnyonge);

g) Fasihi si chochote isipokuwa mdundiko wa kujistarehesha na kujisahaulisha matatizo.

3. Kwa maneno machache, mwandishi wa makala hii anasema kuwa kazi kuu, na huenda pekee ya fasihi ni kuburudisha. Dhima nyingine zaidi ya hiyo, kama alipata kuisema au kuishabikia hapo nyuma, ama kusemwa na mtu mwingine, basi tangu sasa anaibatilisha.

4. Madai hayo ya mwandishi wa makala yana uzito, na inaelekea yanaweza kuwa ni chanzo cha mjadala mwingine mkali wa kifasihi ili kuendeleza kidogo kuzizamia dhana za fasihi, ubunifu, ujumi na sanaa. Hata hivyo, suala la mtaalam kuwa na mtazamo huu leo juu ya dhana fulani, na kesho akabadili msimamo wake na kuitazama dhana hiyohiyo vinginevyo, si geni. Aliyevuma sana mwanzoni mwa karne hii ni yule mwanafasihi maarufu wa Kirusi, Leo Tolstoi, huenda baada

ya uzee kuanza kumtamirira na kuona kiza cha mustakabali wake kikimnyemelea, aliuacha mkondo wa kimapinduzi wa kikomunisti na kuwa muumini wa kidini. Naye TSY Sengo (1993) akimjadili mhakiki anayefaa alidai kuwa mhakiki anayebadilishabadilisha misimamo yake ndiye anayefaa, ilimradi tu aweze kutetea hoja zake. Sijui kama mwandishi wa makala hii anasibiwa na hali ile ya Tolstoi au ya Sengo. Hebu tumrejelee kidogo.

4.1. Mwandishi wa makala anapodai kuwa fasihi haiwezi kubuni, bali huunda ulimwengu kutokana na ule uliopo anadhani anakuwa umbali gani kutoka kwa akina Nkwera na Ramadhani ambao wanadai kuwa fasihi huchota tu kutoka kwenye hazina ambayo tayari ipo? Je, huo siyo u-Tolstoi?

4.2. Eti fasihi si chochote isipokuwa ni `mdundiko wa kujistarehesha na kujisahaulisha matatizo'! Ni kweli kabisa kwamba kazi mojawapo ya msingi ya fasihi ni kuburudisha au kustarehesha. Lakini kazi nyingine ambayo hali kadhalika ni ya msingi ni kwamba ndani ya burudani hii na starehe hii aghalabu huwa kumesheheni ujumbe. Tafiti kadhaa zimefanywa kuhusu suala hili. Mathalani, tuone mfano mmoja katika fasihi-simulizi za Wazulu. Landeg White amefanya utafiti wa muda mrefu katika jamii kadhaa za kusini mwa Afrika. Alipofanya utafiti kuhusu Izibhongo (mashairi marefu ya Kizulu), alibaini jinsi ambavyo watu wa kawaida na askari walivyotumia mashairi hayo kumwambia Mfalme wao matatizo yao. Wafalme kama vile Chaka, pamoja na kali wao, walipozwa hasira zao na mashairi haya na kupata kusikiliza matatizo ya watu wao na kuyashughulikia pale ilipowezekana. Hali kadhalika, viongozi wa namna hiyo (yaani Watemi na Wafalme), aghalabu walikuwa na `msemaji' wao ambaye kwa Kiingereza aliitwa `clown'. Huyu alikuwa ana macheche mengi, aliyejawa vichekesho, nyimbo, vitendawili, methali na mizungu mingine ya kumfurahisha mkuu wake. Yeye alikuwa na kazi kubwa ya kumshauri, kumtahadharisha na kumtanabahisha mkuu wake. Watu wa kawaida na hata viongozi wa ngazi za chini walimtumia sana mtu huyu kuwasiliana na mkuu wao wakati wa matatizo. Chifu Mukwava alikuwa na mtu kama huyo. Wafalme wengine, hususan wa Afrika Magharibi walikuwa na mayeli. Dhima ya fasihi-andishi ni ya wazi zaidi, isipokuwa pale ambapo msanii huenda hakuifanya kazi yake vizuri. Katika mazingira ya namna hiyo utaona kuwa hata upande wa burudani huweza kupwaya pia.

4.3. Je, mwandishi ana maana gani anaposema kuwa fasihi haiibui jipya lolote? Huenda angekuwa msaada mkubwa kama angefafanua kwanza ana maana gani na dhana hiyo ya upya; kisha akatueleza ni uwanja upi tu wenye uwezo wa kuleta mapya? Mwandishi anapokubaliana na mawazo ya Lenin aliyeshauri fasihi isitazamwe katika hali halisi tu (*concrete situation*), bali akahimiza watu waote ndoto, anadhani alikuwa na maana gani hapo? Mimi nadhani Lenin alikuwa anapanua mipaka ya ubunifu, kwa maana kwamba wasanii waihimize jamii katika mwelekeo wa `upya'. Jules Verne, yule mwandishi wa Kifaransa wa hadithi za mwezini na katikati ya dunia, alitoa mchango maridhawa katika kuleta mapinduzi ya kifikra juu ya maisha ya anga za mbali na katika moyo wa ardhi...Wasomaji wengi wa kazi zake, isipokuwa Senkoro waliona namna mpya ya kifikra ambayo ililetwa na msanii huyo katika uga wa fasihi. Hali kadhalika, msanii wa hivi karibuni, Euphrase Kezilahabi, amejitokeza na kazi zake za **Nagona** na **Mzingile** ambazo ni namna ya kazi ambazo bado hazijazoeleka katika uga wa fasihi ya Kiswahili. Zina `ugeni' fulani ambao umeleta gumu fulani kwa baadhi ya wasomaji wake katika kuifikia maana. Ugeni huo unafumbata upya fulani katika usanii wa msanii huyo ambao ameuleta katika fasihi ya Kiswahili. Kwani maana ya upya ni nini kama si ile ya `kuona' kwa mara ya kwanza au `kuona' kwa namna nyingine ambayo hukuijua. Dunia imejaa mambo mengi ambayo tunaendelea kuyafunua au kufunuliwa na wengine kwa njia ya utafiti, ugunduzi na majaribio, pamoja na bahati nasibu na

ajali. Zote hizo ni baadhi ya njia za kuleta mambo mapya. Vinginevyo, Senkoro afute dhana ya `upya' kama inavyofahamika, na atuletee dhana nyingine muafaka zaidi.

5. Karibu masuala yote ambayo yamehojiwa na mwandishi wa makala yana majibu, ijapokuwa kila anayejibu haiyumkini atakuwa na mtazamo wake. Mfano mzuri ni ule wa vipofu sita waliokwenda `kumwona' tembo, na kila mmoja akagusa sehemu fulani ya mwili wa tembo. Je, ni kipofu yupi alisema uongo? Na yupi kati yao alisema kweli? Katika fasihi, na hata fani nyingine nyingi hususan za Sayansi za Jamii, sisi sote ni vipofu ambao tunaifukuzia `kweli' kwa kasi za kuachana na uono wa kuachana. Mmoja ameshikilia mguu wa `kweli' akadhani ameishikilia `kweli nzima'; mwingine ameshikilia sikio la `kweli', na mwingine ubavu, na mwingine mkono, na hali kadhalika. Kila mmoja wao anadhani ndiye ameishika `kweli yote'. Tofauti hizi za `kuona' na `kuishika' kweli ndizo zinatufanya tutetane na hata kugombana. Lakini swali kuu linabaki palepale: aliye sahihi ni nani? Na mkosa ni nani? Sipendi kujaribu kulijibu kila swali hapa, kwani nitakuwa ninaandika makala mengine. Kijisehemu hicho cha 4 hapo juu kimetosha kama dokezo.

6. Masuala madogomadogo ya kuangaliwa ni pamoja na:

- Wananadharia Waswahili wa mwanzo maana yake nini? Nini kiliwafanya wafikiri kwamba mjadala umefungwa?(uk.1)

- Je, ni kweli kwamba katika uchongaji lugha kuu ni gogo?

- Katika uk.3 aya ya 2, nadhani swali halijawekwa vizuri. Msomaji mwingine anaweza kudhani hakuna swali kwa sababu tayari lina jibu. Sababu ni kwamba baadaye mwandishi wa makala anakuja kulijibu hilo swali kwa kubadili tu jina. Badala ya `ghibu' linakuwa `umbuji'.

- Sijaona sababu za msingi za mwandishi kuikana maana ya pili ya Senkoro kuhusu sanaa. Maana hii ambayo inaelekea kuwa imeazima kitu fulani kutoka kwenye maana ya akina Mlama na Balisidya si ya jumla kwa kiasi kikubwa mno. Hata hivyo, hatimaye swali la msingi ni kwamba maana zipatikanazo kwa njia ya fafanuzi hutoa mwanga wa jumla juu ya dhana zinazofafanuliwa. Fafanuzi za namna hiyo dhima zao ni kudokeza tu dhana inayohusika, na wala si kuaridhia `a-z' ya dhana hiyo.

- Mwandishi anauliza kama hotuba ni fasihi. Arejee **Mulika Na.21** na kuisoma makala ya M.M.Mulokozi kuhusu tanzu za Fasihi Simulizi na kuona jinsi kipengele cha hotuba kinavyotazamwa.

- Je, ni kweli kwamba sanaa za asili `si ubunifu wa kiurazini'? Je, maumbo ya masega ya nyigu na nyuki ni ya bahati nasibu? Je, umbo zuri la ua lenye nektari ambayo hatimaye inanasa wadudu wakawa ni mlo wa mmea ni suala la bahati nasibu? Tumeyajifunza mambo hayo kiasi gani na kuwa katika kutamka tamko lenye mashiko? Kuna utafiti mkali ambao unafanywa katika maeneo hayo ili kubaini akili za viumbe wa ardhini, hewani na majini ambao awali tulidhani wanaishi kwa hisia za kibayolojia tu. Lakini vilevile kuna masuala

kama vile upinde wa mvua ambao inaweza kukubalika kuwa rangi zake ni tokeo la bahati nasibu tu ambalo linaelezeka kisayansi.

- Kuhusu kazi ya kitanzia, mwandishi anadai kuwa haiwezi kuwa na lugha `yenye kuburudisha', bali `mvuto wa kiumbuji'. Je, mvuto wa kiumbuji una dhima gani kama si hiyo ya kuburudisha? Je, unapokwenda kuangalia tanzia ya Mukwava jukwaani, lengo lako ni kwenda kuomboleza na kuogopeshwa? Au ile ya Julius Kaizari? Unapojinasibisha na mchezaji wa kabumbu kama vile Pele, ukaishia pale ulipokaa, na hatimaye anapofunga goli, na wewe katika sehemu yako ukapiga teke kiti au mtu ukimsaidia Pele kufunga goli bila kujijua, hiyo ni sanaa. Vivyo hivyo Iago anapofanikiwa kutumia uzandiki wake kumlaghai Othelo - kipenzi cha mtazamaji - akalaghaika. Chuki ile ndani yako ni zao la ushindi wa msanii katika kumteka msomaji wake na kumfikisha kwenye `carthasis'.

- Je, saa ya ukutani inataka kutusaidiaje? Je, ndivyo wataalam hawa waionavyo saa? Au unalinganisha saa na kazi ya fasihi inavyoangaliwa na watu hawa?

- Hatimaye ni kuhusu ufafanuzi wa dhana ya ubunifu. Mwandishi amekataa kuwepo kwa upya; lakini katika ufafanuzi anaonyesha kuwapo kwa upya huo. Je si kupingana huko?

7. Mwisho, makala hii ni changamoto nzuri katika kuamsha mawazo yaliyolala au yanayoelekea kusinzia kuhusu dhima ya fasihi katika jamii.